# MWONGOZO PP3

**1. a) Tambua kipera cha Fasihi Simulizi kinachohusishwa na kifungu hiki.** **(ala. 2)**

Mawaidha

**b. Jadili sifa nane za kipera hiki.** **(ala. 8)**

- Ni mawazo mazito kuhusu maisha k.v unyumba, urithi, mapenzi, malezi, n.k
- Mawaidha hulenga hadhira maalum
- Hulenga maudhui maalum
- Huibua maadili yanayohitajika kuzingatiwa
- Ujumbe katika mawaidha hujitokeza moja kwa moja
- Hutolewa na mtu mmoja anayeaminika kuwa mjuzi wa anayezungumziwa
- Hutumia lugha ya kipekee yenye maana ya kina, na ya kuvutia hadhira
- Tamathali nyingi za usemi hutumiwa.

**c. Jadili vipengele <u>vinane</u> vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi** **(ala. 8)**

- <u>Dhamira</u>: Ni lengo au nia kuu inayokusudiwa kuwa; kuadilisha, kuonya, kuelimisha au kukashifu.
- <u>Maudhui</u>: Ni jumla ya mambo yanayoelezwa katika hadithi k.m. ujanja / ulaghai n.k.
- <u>Ploti</u>: Mtiririko wa matukio katika hadithi kulingana na jinsi yanavyosababishana.
- <u>Mandhari</u>: Haya ni mazingira ya wakati, hali au kimaeneo ambayo yaweza kuwa ya kuogofya
- <u>Wahusika</u>: Ni viumbe wanaoshiriki katika hadithi ambao wanaweza kuwa binadamu, wanyama, mazimwi au vitu visivyokuwa na uhai.
- <u>Muundo</u>: Hadithi huwa na muundo maalum wa ufunguzi, mwili na hitimisho.
- <u>Lugha</u>: Hadithi hutumia lugha ya moja kwa moja ingawa huweza kuwa na tamathali kama methali, tashbihi, jazanda, usambamba n.k.
- <u>Funzo:</u> Hadithi nyingi hutoa funzo fulani la kimaadili k.m. wizi haufai au wajanja hatimaye huangamia.

**d. Jadili sifa mbili za vitanza ndimi** **(ala 2)**

Hutamkwa kwa kasi

Sauti hukaribiana kimatamshi- Wali huliwa na mwana wa liwali. Asiyekuwa mwana wa liwali hali wali wa liwali.

Kuna uradidi wa sauti fulani- Shirika la reli la Rwanda lililiathiri lile la reli la Kenya.

**SEHEMU YA B**

2. a) Muktadha wa dondoo
- ni kauli ya Imani
- akimsemea Amani.
- Punde baada ya sherehe ya amu yake Amani kuachiliwa huru,Imani anamshajisha Amani kuandika tawasifu yake.
- Anamrai awasawiri vilivyo wanawake katika tawasifu ile. (alama 4x1=4)

b) Mbinu za uandishi.
- Nahau- usiniweke pembeni

- Tashbihi – kama tanbihi (alama2x1=2)

c) Usawiri wa Wahusika wa kike.

- Kuna wale wenye utu- Imani na Zuhura.
- Wasioridhika Michelle,
- Wenye mapenzi ya dhati- Mashaka.
- Walezi wema – Imani na Zuhura.
- Waasherati kama Lowela.
- Waadilifu kama Imani na mama yake.
- Wanaowajibika kazini kama Imani na mama yake.
- Jasiri- Imani na kwa kiwango fulani, Dora.
- Wengine wanaonekana kuishi kwenye vivuli vya wanaume
- Wasiomakinika –msichana aliyetungwa mimba na Fao
- Wasiosoma- bi kizee
- Wavumilivu-zuhura

(alama 7x2=14)

3. Katika nchi ya Tomoko, uhuru ni ndoto ambayo bado haijatimia.Jadili.

- Nchi ya Tomoko iliwahi kutawaliwa na waliodhulumu wenyeji – waliyatwaa mashamba yao, wakawakataza kufuga au kupanda mazao yaletayo fedha.
- Walishurutishwa kuwafanyia walowezi hawa kazi huku wakiishi katika mabanda.
- Walio mamlakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
- Waafrika walipochukua hatamu za uongozi mambo hayakubadilika . Walio mamlakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
- Mashamba yao yanatwaliwa mfano shamba la Chichiri na Mwinyihatibu.
- Wanafungwa jela kwa visingizo kama vile Yusuf na Amani.
- Vyombo vya Dora vinatumiwa kuendeleza matakwa ya watawala.
- Wanyonge wanafanyizwa kazi za kijungu jiko
- Lugha ya kikoloni ndiyo inayopendelewa nawatawala hawa weusi.
- Hawana uhuru wa kujiamulia mambo – Imani anatishwa na askari kwa kutohudhuria sherehe.Wananchi wamejazwa uoga.
- Ukosefu wa huduma muhimu kama vile matibabu.
- Uhuru wa kunena haupo mfano Matuko Weye anawekwa seli kwa kauli yake.
- Ukabila na ukoo unatumiwa katika kugawa nyadhifa na kazi – Nasaba Bora alipewa cheo cha utemi kwa upendeleo.
- Kitoto Uhuru ni ishara ya uhuru usio kamili , usiotunzwa na waliopewa jukumu la kuutunza.kufa kwake ni ishara ya utovu wa uhuru kamili.
- Ndoto huenda itatimia baada ya ukombozi wa pili ulioongozwa na Madhubuti na Amani.Madhila yatakomeshwa na haki kudumishwa.

(alama10x2=20)

**SEHEMU C, Tamthila: Kigogo**

4. i) Maneno haya yalisemwa na Kenga.

ii) Alikuwa katika karakana ya uchongaji vinyago.

iii) Alikuwa akimzungumzia Sudi

iv) Sudi anaonesha kutokubaliana na mradi uliofadhiliwa wa kuchonga kinyago cha Ngao.

**b) Umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia**

Mhusika ni muhimu kwani ni kielelezo cha;

i. Watu ambao wanateuliwa katika wadhifa muhimu lakini wanakosa kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa. Yeye aliteuliwa kuwa mshauri mkuu na binamu yake Majoka. Lakini ushauri wake mmbaya unachangia kuporomoka kwa uongozi wa Majoka. Kwa mfano, anashauri kufungwa kwa vyombo vya habari na kubaki kwa kituo kimoja ambacho kitasifia utawala wa Majoka.

ii. Wasaliti- Majoka alimwamini sana kama mshauri wake mkuu, lakini mambo yanapochacha, anamsaliti Majoka na kuungana na utawala mpya.

iii. Viongozi ambao hutenda kazi chini ya mwavuli wa tamaa. Anamshauri Majoka wafunge soko la Chapakazi huku akitarajia kupewa kipande cha ardhi ya soko hilo.

iv. Viongozi ambao hunufaika na rasilmali za nchi na kuwatenga walio wengi.

v. Viongozi wafisadi- Kenga anakubaliana na serikali ya Majoka ili wanajamii waongezewe kodi,badala yake kutetea maslahi ya wanyonge kama mshauri mkuu wa serikali.

vi. Viongozi wakatili- Kenga anafurahi anaposikia kuwa vijana watano wamepoteza maisha yao katika maandamano. Vilevile anashiriki katika kupanga njama za kumwangamiza Tunu na Chopi, mlinzi wake Majoka ambaye wanahofia anaweza akafichua siri za utawala wa Majoka

vii. Kuwa viongozi wabaya hawawezi wakadumu mamlakani licha ya juhudi zao.

**c) Kauli inavyoafikiana na matukio katika tamthiliya ya kigogo.**

i. Dawa ya deni kulipa ni methali inayoeleza kuwa katika vitendo vovyote vile ambavyo binadamu hutekeleza, lazima viwe na malipo kwa njia moja au nyingine.

ii. Majoka katika utawala wake wenye dhuluma nyingi na maovu anawakandamiza wanasagamoyo wengi na mwishowe wanamwondoa mamlakani. Umma unaonesha kuwa na hasira na unajongea mbele kumvamia lakini walinzi wake wanawazuia.

iii. Kupitia kwa mazungumzo ya Majoka na babu, twaona Majoka akilipa deni la uongozi wake mmbya kwa kusumbuka na kutokuwa na amani katika nafsi yake. Majoka anana

ziwa la damu huku mikono yake ikiwa imefungwa nanga ndani ya damu hiyo. Kuna kilio cha ndani kwa ndani pamoja na machozi ya rangi ya damu. Majoka anaonekana kutokuwa na amani. Sauti ya Jabali na watu wengine waliouawa chini ya uongozi wake zinamtia adha na kumnyima utulivu.

iv. Majoka amemiliki kampuni ya kutengeneza sumu ya nyoka almarufu kama dawa za kulevya. Anajitajirisha kutokana na kuharibu watoto wa watu kwa dawa hizi. Dawa hizi zinatumika hata na wanafunzi katika shule yake ambao wanageuzwa kuwa makabeji. Deni hili la kuharibu watoto wa wengine linalipwa wakati ambapo mwanawe Majoka Ngao Junior anafia uwanja ndege kutokana na athari za dawa za kulevya.

v. Ngurumo alikubali kutumika na Majoka kuendeleza kila aina ya ukatili kwa wanasagamoyo. Anasaidiana na genge kuhangaisha wale wanaoshukiwa kuwa wapinzani wa Majoka. Analipa deni hili la kufanyia wanasagamoy ukatili kwa kunyongwa na Chatu ambaye Majoka alikuwa ammemfuga na kuzikwa kama mnyama.

vi. Mamapima amenufaika na utawala dhalimu wa Majoka kwa kupata tenda ya kuoka keki ya Uhuru ingawa kimagendo na kupewa kibali cha kuuza pombe haramu inayoua na kupofusha wanasagamoyo. Wakati Majoka anapopinduliwa, anasikika akilia kuwa anawindwa. Wakati wake wa kulipa deni la kuwauzia pombe haramu wanasagamoyo unafika. Pombe yake inamwagwa na anasakwa ndipo aweze kukabili mkono wa sheria.

vii. Chopi, mlinzi wake Majoka naye anaishi kwa kutekeleza amri za bwana wake za kuwafanyia wanasagamoyo ukatili. Alishirikiana na majambazi wengi kumvamia Tunu, mpinzani wa Majoka wakiwa na nia ya kumwua. Tunu anaponea chupuchupu lakini wanamwacha kama wamemvunja mguu. Hata hivyo, Chopi analipia deni hili kwa Majoka na Kenga kukubaliana kumwua kwa kuwa anajua siri nyingi za utawala wa Majoka na walihofia angezitoa nje pindi utawala mpya ukichukua hatamu za kuongoza.

viii. Wazalendo kama Tunu na Sudi wanateseka wakitafuta ukombozi wa Sagamoyo. Tunu anavamiwa na kuvunjwa mguu. Ashua, mkewe Sudi anatiwa ndani kama njia ya kumvunja moyo Sudi na kumfanya kuwa mfuasi wa Majoka. Juhudi zao zinazaa matunda na inatarajiwa watalipa deni na kuongoza kutafuta ukombozi wa Sagamoyo kwa kuchukua hatamu za uongozi.

**5. Mbinu ambazo Majoka anatumia kujidumisha mamlakani**

i. Mauaji. Majoka anawaangamiza wapinzani wake. Utawala wake uliangamiza Jabali, mpinzani wake mkuu katika ajali ya kupangwa.

ii. Kuzima maandamano. Wanasagamoyo hawana sauti ya kulalamikia haki zao pamoja na ukiukaji wa sheria na viongozi. Wanapojaribu kufanya hivyo, utawala unajibiza kwa kutumia mabavu na kuua pamoja na kulemaza waandamanaji.

iii. Vitisho. Utawala wa Majoka unawatumia vitisho ili kuendelea kujidumisha mamlakani. Majoka anatumia vitisho ili kuwanyamazisha wapinzani wake. Bi Hashima anaeleza Siti kuwa wametiwa woga na wanaishi kwa hofu. Boza anamtahadharisha Sudi kuwa hawezi kushindana na Kigogo . Kenga naye anampa Sudi onyo kuwa atahadhari na ulimi wake usije ukamtia matatani. Utawala huu unapomtia Ashua mkewe Sudi ndani unampa kitisho kuwa asipokichonga kinyago cha Kiongozi, hawatamwachilia mkewe.

iv. Dhuluma na ukatili-Majoka anwadhulumu watu wengi ikiwemo Ashua. Anamsingizia Ashua kuwa amezua vurugu ofisini mwake. Ashua anatiwa ndani na kupigwa dhidi ya vidole vyake kufuja damu. Utawala wa Majoka una genge la vijana wanaotumiwa kuwafanyia raia kila aina ya ukatili na dhuluma. Kundi hili likiongozwa na Chopi linamvamia Tunu ambaye ni mtetezi wa haki kwa nia ya kumwangamiza. Matoke yake ni kumvunja fupa la mguu.

v. Matumizi mabaya ya vyombo vya dola. Utawala wa Majoka unawatumia askari vibaya katika kuwatia hofu wanasagamoyo. Jeshi la polisi hupewa amri za kutumia vitoa machozi na hata kuwaua pindi utawala unapohisi kuwa kuna tisho fulani miongoni mwa wanasagamoyo.

vi. Vyombo vya habari. Kuna vyombo vya habari kama redio vinavyotumiwa na utawala kueneza propaganda zinazolenga kusuga wanasagamoyo akili kwa manufaa ya utawala. Kwa mfano, habari zinapeperushwa katika redio kuwa Wanasagamoyo watakuwa na mwezi mzima kusherehekea na kuchangamkia ufanisi wao wa miaka sitini ya uhuru wao. Kwa upande mwingine, vyombo vya habari ambavyo vinaonekana kutopeperusha habari zinazochangia kusuga watu akili kama kituo cha runinga cha Mzalendo vinafungwa. Hii ni katika juhudi za kuhakikisha kuwa wanasagamoyo hawapati habari kamili kuhusu

serikali yao. Aidha Majoka anaghadhabika kwa kuwepo mitandao ya kijamii ambayo inasambaza habari hasi kumhusu kwa urahisi na wepesi.

vii. Mbinu ya tenga-tawala. Utawala wa Majoka unatumia mbinu ya kutenganisha. Inajaribu kuwatenganisha Tunu na Sudi ili kusambaratisha nguvu za kutetea ukombozi. Utawala unatoa hongo kwa wafanyakazi wenzake Sudi ili kuwazuia kushiriki katika harakati za ukombozi. Kombe anahongwa kwa kipande cha keki ili asiungane na wapinzani kama Sudi.

viii. Matumizi ya dawa za kulevya na pombe haramu. Majoka ana kiwanda kinachosifika barani Afrika kwa utengenezaji wa sumu ya nyoka almaarufu kama dawa za kulevya ambazo zinatumiwa kuwafanya vijana makabeji yasiyo na uwezo wa kupinga utawala dhalimu wa Majoka. Mamapima apewa kibali cha kuuza pombe haramu. Pombe hii inanywesha vijana ambao hawajijui hawajtambui. Baadhi wanasikika wakidai kuwa kura zao hawampi mtu mwingine isipokuwa Majoka. Ngurumo anasema kuwa afadhali ampe paka iwapo si Majoka.

ix. Hongo. Utawala wa Majoka unahonga baadhi ya wanajamii ili kuhakikisha kuna wafuasi. Hawa ni pamoja na wanaopewa kibali cha kukata miti, akina Kombe ambao wanapewa kipande cha keki ya uhuru. Kenga naye anaoekana kumwuunga mkono Majoka kutokana na vitu anvyopata kama kile kipande cha ardhi anachotarajia kutoka soko la Chapakzi.

x. Utoaji wa elimu duni. Elimu inayotolewa Sagamoyo haiwezeshi wanaoipata kupata maadili, maarifa na hisia za kizalendo. Ni elimu duni ambayo inawafanya kuwa makabeji yanayofuata utawala mbumbu kama mzungu wa reli.

xi. Matumizi ya propaganda. Propaganda zinaelezwa kuwa siasa za wanaharakati zinalenga kugawanya wanasagamoyo na kurudisha maendeleo yaliyopatikana nyuma. Majika anawatahadharisha wanasagamoyo kutofuata wanarakati hawa.

6. i) Ni kauli ya msimulizi wa hadithi.

ii) inamrejelea Samueli, mwanafunzi aliyehitimu kidato cha nne.

iii) Samueli yuko katika faragha ya msalani pale shuleni alikoingia pasi na kusukumwa na haja.

iv) Hii ni baada ya kurushiwa matokeo na mwalimu mkuu na kuona kuwa amefeli mtihani.

**(b)** Samueli ni;

i. **Mwoga**. Anaonesha uoga anapoingia katika ofisi ya mwalimu mkuu na anapoongea nae anasitasita ishara ya kuwa mwoga. analemewa kuwakabili wazazi wake na kuwaeleza kuwa amefeli mtihani. Anatetemeka pia anaomwona baba yake pale bawani alipojitoza ili afe.

ii. **Mwenye majigambo**. Anajigamba kuwa ana hakika atapita mtuhani na kumshtua mwalimu mkuu ambaye alionesha kutokuwa na imani naye. Anazi kujitapa kwa kudai kuwa anaelewa yeye si mwerevu sana. Lakini huweza kupanga mambo yake na kile asomacho ndicho hutokea katika mtihani. Alijitapa kwa mpenzi wake Nina kuwa yeye ni bingwa wa masomo.

iii. **Mwongo**. anahadaa baba yake kuwa hakupata matokeo kwa kuwa hakuwa amekamilisha kulipa karo.

iv. **Mwenye bidii**. Anasema alikuwa akitembea mwendo wa kilometa sita kwenda shuleni kila siku na kuwa alihudhuria madarasa yake vizuri.

v. **Bwege**. Kutokana na majibu ya yale ambayo anasema anayajua, aonesha kuwa zuzu na si ajabu alifeli mtihani.

vi. **Mcheshi.** Anachekesha kwa kauli yake kuhusu mwalimu mkuu na wazazi wake. Anasema kuhusu Mwalimu mkuu, "*Labda Mwalimu mkuu kazidiwa na maumivu. Labda anataka kufanyiwa operesheni ya ubongo ama anahitaji maombi hasa atakuwa na akili razini tena*". Kuhusu wazazi wake anasema, " …mama na baba wameumbwa kwa aina tofauti za udongo."

vii. **Mwepesi wa kukata tamaa**. Kufeli mtihani shuleni anaona kana kwamba amefeli maishani. hii ndiyo sababu anaamua kujiua.

**(c)** i) Anasumbuliwa na kufeli mtihani. Anaona juhudi zake nyingi za kutembea kilometa sita kwenda shuleni na kuwa na mahudhurio mazuri darasani zimeshindwa kuzaa matunda.

ii) Analemewa na vipi alivyofeli mtihani ilhali kuna mambo aliyoyajua na alihudhuria madarasa vizuri.

iii) Anaona muda wa miaka minne, karo iliyolipwa na baba zimepotea.

iv) Anashindwa kama kuanguka mtihani ina maana kuwa hajui lolote.

v) Anaona kuwa baba yake hataelewa akimwambia kuwa amefeli mtihani.

vi) Anaona kama amesaliti wazazi wake ilhali yeye kama mwana wa kiume wa peke ndiye tegemeo lao la kuwakwamua katika lindi la uchochole.

7. a) Muktadha wa dondoo:

i. Ni kauli ya mwandishi

ii. Kumhusu Otii

iii. Wako kwenye chumba cha Otii

iv. Hii ni baada ya mwenyekiti wa chama cha watu wa nyumbani kupinga kauli yake ya kuwataka kumzika pale Mombasa atakapokufa badala ya kusafirisha mwili wake kwao nyumbani Sidindi karibu na Kisumu .

b) Tamathali iliyotumika hapa ni tashbihi.inatumika ili kuonyesha hali ya kupuuza ya wanachama wa umoja wa watu wa nyumbani. Wanapuuza rai ya mgonjwa kuwa azikwe pale Mombasa . Kulingana nao rai yake si lolote si chochote na yapaswa kupuuzwa. Otii analinganisha hali hii na maji ya moto ambayo hayana uwezo wa kuchoma nyumba.

ch) Sifa za wanaorejelewa; Hawa ni wanachama wa chama cha umoja wa watu nyumbani.

- **Ni wenye mapuuza**. Wanapuuza kauli ya Otii ya kutaka kuzikwa Mombasa anakoishi na atakakofia.
- **Wakereketwa sugu wa mila na tamaduni za jamii**. Mwenyekiti wake anasema kuwa hawawezi kukiuka mila na ada zao kwa kumwachia mwenzao kutupiliwa mbali kana kwamba hana kwao.
- **Wenye utangamano.** Wameunda chama cha watu wa asili moja chenye lengo la kusaidiana wakati wa changamoto. Wanajitolea kuchangisha pesa za kununua jeneza, mavazi ya kumvisha maiti na za kugharamia uchukuzi wa maiti na waombolezaji. Wanajitokeza kwa wingi hadi chumba cha Otii kinafurika.
- **Wakarimu kwa mmoja wao.** Wanajitolea kuchangisha pesa kwa ukarimu.
- **Wajeuri**. Wanajadili mipango ya mazishi mbele ya mhusika ambaye wameambiwa na daktari kuwa anaweza kuaga dunia wakati wowote. Hawajali athari za majadiliano yao kwa mhusika.
- **Wabadhirifu.** Kutokana na hali yao ya kushikilia utamaduni, wanatumia kiasi kikubwa cha fedha kusafirisha maiti, waombolezaji na kununua mavazi ya kuvika maiti. Anayejadilia anawatahadharisha na kuwarai wamzike pale Mombasa lakini wanakataa kata kata.

d) Dhima ya anayedokezwa katika kauli;

Huyu ni Otii, mhusika. Yeye kijana barubaru ambaye alikuwa mchezaji hodari wa soka. alichezea Bandari F.C na timu ya taifa Harambee Stars. Umuhimu wake katika hadithi kuwa;

i. Ni kielelezo cha vijana wenye vipawa ambavyo haviwasaidii. Ana kipawa cha kucheza kadanda. Badala ya kutumia anachopata kwa njia inayofaa, anakitumia kwa starehe ambazo zinamchongea.

ii. Anawakilisha vijana wenye sifa, wapenda anasa na burudani. Anapenda kwenda kwenye vilabu kustarehe.huko ndiko alikopata Rehema Wanjiru, msichana ambaye anatuhumiwa alimwambukiza UKIMWI.

iii. Ni kiwakilishi cha vijana wenye tamaa, uchu na wazinifu. Aliwapenda wasichana warembo na hata anapotahadharishwa anatetea hali yake kwa kusema kuwa nzi hufia

kidondani si haramu. Kwa kweli, hapo ndipo nzi anastahili kufia akitafuta riziki. Ngono si riziki.

iv. Anatumiwa na mwandishi kuonesha vile utepetevu wa viongozi. Viongozi wa michezo wanaoneshwa kutowajali wachezaji hasa wanapopatwa na msiba. Viongozi wa Michezo walimtelekeza Otii wakati alipopata maumivu gotini na alipougua UKIMWI.

v. Ni kielelezo cha watu katika jamii wanaoridhika na hali wanazojipata kwazo. Otii anaridhika na mshahara mdogo anaopata pale bandarini baada ya kuumia. Anatosheka pia na hali duni ya mastakimu yake.

vi. Anatumika kuonesha watu wenye tabia ya mapuuza katika jamii.
- Anapuuza tahadhari anayopewa na rafiki yake dhidi ya wasichana warembo.
- Anapuuza kwa kutetea tamaa na matamanio yake kuwa nzi hawezi akalaumiwa kufia kidondani. Pale ndipo anapopata riziki yake.

vii. Anaonesha wanajamii ambao wanasahau na kupuuza mila na tamaduni za jamii zao. Otii haoni haja ya kwenda kuzikwa mbali na pale alipofia. Yuko radhi kwenda kinyume na desturi za jamii yake kuwa mtu akifa azikwe nyumbani. Yeye angetaka azikwe pale alipokufia

8. a). **Sifa tano**
- Hodari wa kufanya kazi / wenye bidii / wakulima hodari / hawatulii hadi wapate.
- Wenye kujiamini
- Waliopuuzwa / hawana makubwa- hawasikiki
- Hawana tamaa
- Wenye kupinga ulaghai / wa kweli
- Wenye ndoto / ndoto haizimiki
- Hawahini / huwapa watu haki yao / waaminifu
- Wazalendo
- Wanaohangaika / wanaoteseka kupata / wanaosumbuka

a) **Umuhimu wa tamathali tatu**
- Tashbihi-kama watanga na mpini- kuonyesha jinsi walivyojitolea (bidii)
- Tashhisi / uhaishaji- tamaa za moyo kutii, kupigana na ulaghai-hapa tamaa za moyo na ulaghai vimepewa uwezo wa kutenda.
- Nahau / msemo-ndoto haizimiki-hawapotezi tumaini, kuonyesha hali ya kutokata tamaa.
- La haramu watu hawali-kuonyesha hawafaidiki kwa wasichofanyia kazi.
- Taswira-kutwa kile na hiki kama watanga na njia- kuonyesha watu wanaoshughulika kufanya kazi kuiendeleza nchi.
- Sitiari / jazanda-ndoto haizimiki-hawapotezi tumaini.
- Taashira-watokwa jasho vijijini-bidii
- Kinaya-japo wasikia hawakosi kujiamini -kuonyesha kutokata tamaa.-(kutaja 1, umuhimu 1).

b) **Mbinu za kutosheleza mahitaji ya kiarudhi-**
- Mazida-vinyuani badala ya vinywani ili kutosheleza mahitaji ya idadi ya mizani.
- Kufinyanga sarufi / kuboronga sarufi / miundo ngeu ya kisintaksia / ukiushi wa kimuundo k.m.tamaa za moyo kutii, badala ya kutii tamaa za moyo

- La haramu jasho hawali, badala ya hawali jasho la haramu
- Ya kesho kuwa hali njema badala ya hali ya kesho kuwa njema-imetumiwa kupata urari wa vina.
- Udondoshaji wa maneno (kuacha neno) kama, wiki baada wiki badala ya wiki-umetumiwa ili kutosheleza idadi ya mizani / kupunguza idadi ya mizani.
- Utohozi-wiki badala ya juma.

**c) Kuainisha kwa kuzingatia**

**i) Idadi ya mishororo**

Tathlitha / wimbo / utatu- mishororo mitatu katika kila ubeti.

**ii) Mpangilio wa vina**

Ukara-vina vya kati / ndani vinafanana katika shairi nzima, vya nje vinatofautiana.

**iii) Mpangilio wa maneno**

Kikwamba-kila ubeti unaanza kwa kirai / maneno, mfano-watafuta riziki